

0757478868

2026 KISWAHILI GREDI YA TATU - MUHULA WA TATU

WIKI 1

Somo 1

SHU LE	ENEO LA SOMO	GRE DI	IDA DI	MUD A
	Kiswahili	3		

MADA KUU: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA: (Ndege Nimpenda)

MADA NDOGO: Masimulizi

MATOKEA MAALUM YANAYOTARAJIWA: Kufikia mwisho wa somo mwanafunzi aweze:

- Kutaja aina za ndege wa nyumbani.
- Kusimulia kuhusu ndege ampendaye.
- Kusikiliza kwa makini masimulizi kuhusu utunzaji wa ndege wa nyumbani.

SWALI DADISI: Ni ndege gani umpendaye? Unamtunzaje ndege umpendaye?

VIFAA VYA KUJIFUNZIA NA KUFUNDISHIA:

- KLB Early Grade Kiswahili Gredi ya 3 (ukurasa 106-120)
- Picha za ndege mbalimbali
- Chati

MPANGILIO WA SOMO: Wanafunzi watafanya kazi katika vikundi na mmoja mmoja.

UTANGULIZI Mwalimu atawaonyesha wanafunzi picha za ndege mbalimbali (k.m. kuku, bata, njiwa) na kuwauliza wawataje, na hivyo kuanzisha mada ya ndege wa nyumbani.

UPELELEZI WA SOMO Mwanafunzi aongozwe:

- **HATUA YA 1:** Katika vikundi, wataje aina za ndege wanaowajua, hasa wale wanaofugwa nyumbani.

- **HATUA YA 2:** Kila mwanafunzi apate fursa ya kusimulia kuhusu ndege anayempenda zaidi na kwa nini anampenda.
- **HATUA YA 3:** Mwalimu atasimulia kisa kifupi kuhusu umuhimu wa kuwatunza ndege wa nyumbani.
- **HATUA YA 4:** Wanafunzi watashiriki katika mjadala kuhusu jinsi wanavyoweza kuwatunza ndege wanaowapenda (k.m. kuwapa chakula na maji).

HITIMISHO Mwalimu atamuuliza kila mwanafunzi ataje jambo moja alilojifunza kuhusu kuwatunza ndege. Maswali ya mdomo yatatumika kutathmini uelewa.

MAZOEZI YA ZIADA Wanafunzi wachore picha ya ndege wanayempenda na kuileta darasani.

TAFAKARI KUHUSU

SOMO

.....

.....

Somo 2

SHU LE	ENEO LA SOMO	GRE DI	IDA DI	MUD A
	Kiswahili	3		

MADA KUU: KUSOMA

MADA NDOGO: Kusoma hadithi

MATOKEA MAALUM YANAYOTARAJIWA: Kufikia mwisho wa somo mwanafunzi aweze:

- Kutambua msamiati uliotumiwa katika hadithi.
- Kusoma hadithi zinazohusu ndege wa nyumbani.
- Kufahamu hadithi aliyoisoma na aliyosomewa ili kupata ujumbe.
- Kuchangamkia kusoma hadithi ili kuendeleza ari ya kusoma zaidi.

SWALI DADISI: Unakumbuka nini kutokana na hadithi uliyosoma? Ni kwa nini unampenda ndege wako?

VIFAA VYA KUJIFUNZIA NA KUFUNDISHIA:

- KLB Early Grade Kiswahili Gredi ya 3 (ukurasa 106-120)
- Kitabu cha hadithi